

VITU VYENYE KUHARIBU SWAUMU.

1. Kula na kunywa kwa makusudi, au atakapokula kwa kusahau swaumu yake haitaharibika, kwa kauli yake Mtume aliposema:

(Yeyote mwenye kusahau akala au akanya hali ya kuwa amefunga, basi aikamilishe Swaumu yake....) (Ameipokea Imam Muslim:1155).

Katika vitu vinavyofunguza pia ni kufikisha maji kwenye koo kwa kutumia njia ya pua, au kupidisha chakula katika njia ya mshipa, au kuongezewa damu, vyote hivyo vinaharibu swaumu ya mfungaji.

2. Kufanya tendo la ndoa: Wakati akifanya tendo la ndoa mwenye kufunga swaumu yake inaharibika, itamuwajibikia kuikidhi pamoja na kafara ambayo ni kumuacha mtunwa huru, akimkosa atafunga miezi miwili yenyne kufuatana hatafungua isipokuwa kwa udhuru wa kisheria, kama vile za kusherehekeea Eid mbili au siku za Tashreek za kuchinja, au udhuru wa kuumwa, kusafiri sio kwa kusudia kufungua.

Ikiwa atafungua bila ya udhuru hata kama ni siku moja itamlazimu kuanza upya kufunga ili ipatikane neno kufuatana, ikiwa atashindwa kufunga miezi miwili yenyne kufuatana, basi alishe masikini sitini.

3. Kujitoa manii kwa khiyari kwa sababu ya kupiga busu, au kujitoa kwa njia ya mkono au njia nyininge, kufanya hivyo ni kuharibu swaumu itamujibikia kukidhi siku ambazo alifanya hivyo bila ya kutoa kafara, ama kuota na kutokwa na manii mchana wa Ramadhani hakuharibu swaumu.

4. Kutoa damu kwa kupiga hijama au kwa kujitolea damu kusaidia, kunaharibu funga, ikiwa atatoa damu chache kwa ajili ya uchunguzi hiyo haiharibu swaumu, vile vile kutoka damu bila ya khiyari kama vile damu za pua, au jeraha, au kung'oa jino hiyo haiharibu swaumu.

5. Kujitapisha kwa makusudi ama kutapika bila ya kukusudia hakuharibu swaumu.

Ikiwa atafanya vitu hivi na hali ya kuwa anaelewa na kujua basi swaumu yake itaharibika, lakini ikiwa atafanya kwa kusahau swaumu yake haitaharibika.

Ikiwa atakula kwa kutenzwa kwa nguvu swaumu ni sahihi na wala hatailipa.

6. Kutokwa na damu ya hedhi au Nifasi, muda atakapoona mwanamke damu akiwa amefunga swaumu yake imeharibika, kama inavyokuwa kwa mwanamke ni haramu akiwa hedhi au nifasi kufunga na ni juu lake kuzilipa siku ambazo alifungua.